Afya kwanza!

Wasemavyo wananchi kuhusu huduma za afya

1. Utangulizi

Tanzania imepiga hatua kubwa katika maeneo ya huduma za afya na ustawi wa jamii. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, umri wa kuishi nchini Tanzania umeongezeka kwa miaka kumi kati ya mwaka 2005 na 2015, kutoka miaka 55 mpaka miaka 65. Katika kipindi hicho hicho, vifo vya akina mama na watoto vimepungua kwa kiwango kikubwa na kwa haraka zaidi kuliko nchi nyingine kusini mwa jangwa la Sahara. Vifo vitokanavyo na malaria na virusi vya UKIMWI navyo vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, takwimu hizi za kitaifa zinaweza kuficha hali halisi wanayokutana nayo wananchi. Wanaharakati watetezi na watendaji katika sekta ya afya wamekuwa wakieleza kwamba changamoto nyingi katika sekta ya afya zinatokana na ukosefu wa dawa, vitanda, na upungufu wa wataalamu wa afya.

Muhtasari huu umebeba maoni ya wananchi kuhusu huduma za afya na ustawi wa jamii. Wananchi hupata uzoefu gani wanapoenda kupata huduma za afya? Ni muda gani wanasubiri ili kupata matibabu? Je, wanakutana na upungufu wa dawa, vifaa tiba au wahudumu? Je, wale wanaostahili kutibiwa bila malipo wanapata matibabu bure? Wananchi wangapi wana bima ya afya? Na, je wananchi wana uelewa gani kuhusu huduma zinazotolewa na maafisa ustawi wa jamii wa wilaya?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa Sauti za Wananchi ambao huratibiwa na taasisi ya Twaweza. Sauti za Wananchi ni utafiti kwa njia ya simu za mikononi; na wenye uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Zanzibar haihusiki kwenye utafiti huu. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
+255 22 266 4301 | info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

wahojiwa 1,801 katika awamu ya 19 ya kundi la pili la Sauti za Wananchi, kati ya tarehe 11 na 25 Mei, 2017. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna utafiti wa Sauti za Wananchi unavyoratibiwa tafadhali tembelea www.twaweza.org/sauti

Matokeo muhimu ni:

- Wananchi 6 kati ya 10 hutumia vituo vya afya vya serikali kupata matibabu.
- Wananchi 3 kati ya 4 wanasubiri chini ya saa moja kupata huduma.
- Wananchi 3 kati ya 10 wanasema hospitali walizoenda zina vitanda na magodoro ya kutosha kwa kila mgonjwa [kupata kitanda au godoro lake mwenyewe].
- Wagonjwa 7 kati ya 10 walioenda katika vituo vya afya vya serikali miezi mitatu iliyopita wamekutana na upungufu wa dawa na vifaa tiba.
- Idadi ya watoto wadogo, wajawazito na wazee wanaopata matibabu bure imeongezeka tangu mwaka 2016 lakini wengi wao bado wanalipia huduma hizo.
- Wananchi 5 kati ya 6 wanasema wanapopata majeraha kwenye ajali wahudumiwe kwanza kabla ya kupata fomu ya PF3.
- Wananchi 3 kati ya 4 hawazifahamu kazi za maafisa wa ustawi wa jamii.
- Mwananchi 1 kati ya 4 ana bima ya afya, kutoka mwananchi 1 kati ya 5 mwaka 2014.

2. Mambo nane muhimu yanayobeba maoni ya wananchi kuhusu masuala ya afya na ustawi wa jamii

Jambo la 1: Wananchi 6 kati ya 10 wanatumia vituo vya afya vya serikali

Wananchi sita kati ya kumi (61%) hufika kwanza katika vituo vya afya vya serikali pale mtu anapougua ama kuumia. Hii inafanana na mwaka 2016, lakini inaonesha ongezeko kutoka mwaka 2014 na 2015, ambapo chini ya nusu ya wananchi (45-47%) walitumia vituo vya afya vya serikali. Pia wananchi wachache huenda moja kwa moja kwenye maduka ya dawa na maduka ya bidhaa za kawaida kujipatia dawa.

Asilimia 16-20% ya wahojiwa huenda kupata matibabu kwenye vituo vinavyomilikiwa na watu binafsi, makanisa ama mashirika yasiyo ya kiserikali. Idadi hii haijabadilika sana kati ya mwaka 2014 na 2017.

Kielelezo cha 1: Mara ya mwisho wewe au mtu kutoka katika kaya yako kuugua au kuumia, ulifanya/alifanya nini ili kupata ahueni ya ugonjwa ama jeraha? [1]



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili
2015: Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015) ya kundi la kwanza
2014: Awamu ya 16 (Machi 2014) ya kundi la kwanza

Jambo la 2: Wananchi 3 kati ya 4 wanaoenda kupata matibabu husubiri chini ya saa moja

Wananchi watatu kati ya wanne (76%) wanaoenda kupata matibabu katika vituo vya afya husubiri chini ya saa moja kabla ya kuhudumiwa. Mwananchi mmoja kati ya watano (20%) hulazimika kusubiri zaidi ya saa moja. Upo ushahidi unaoonesha kwamba muda wa kusubiri huduma katika vituo vya afya umepungua kidogo ukilinganisha na miaka ya nyuma, ambapo wananchi saba kati ya kumi (70%) walisubiri chini ya saa moja mwaka 2014.

1 Asilimia huweza kutofika 100% kutokana na majumuisho

Kielelezo cha 2: Ni muda gani wewe/mwanakaya wako alisubiri kupata matibabu? (n=1,373)



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili
2014: Awamu ya 16 (Machi 2014) ya kundi la kwanza

Muda wa kusubiri ni mrefu kwenye vituo vya afya vya serikali kuliko katika vituo visivyo vya serikali. Mgonjwa mmoja kati ya wagonjwa kumi (10%) katika vituo binafsi vya afya husubiri zaidi ya saa moja, ukilinganisha na wagonjwa wawili kati ya kumi (22%) katika vituo vya afya vya serikali.

Kielelezo cha 3: Ni muda gani wewe/mwanakaya wako alisubiri kupata matibabu? (n=1,373)



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za wananchi,* Awamu ya 19 (Mei 2017)

Jambo la 3: Wananchi 3 kati ya 10 wanasema hospitali zina upungufu wa vitanda na magodoro

Wananchi watatu kati ya kumi ambao walilazwa ama walimhudumia mtu aliyelazwa mwaka jana (29%) walikuta hospitali zikiwa na uhaba wa vitanda na magodoro kwa kila mgonjwa. Mwananchi mmoja kati ya wanne (24%) walikuta wagonjwa wawili wakitumia kitanda/godoro moja, na mwananchi mmoja kati ya ishirini walikuta zaidi ya wagonjwa wawili wakitumia kitanda/godoro moja.

Kielelezo cha 4: Wagonjwa wangapi walitumia kitanda/godoro moja? (n=712)



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili
2015: Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015) ya kundi la kwanza

Jambo la 4: Wagonjwa 7 kati ya 10 katika vituo vya afya vya serikali wamekumbana na upungufu wa dawa na vifaa tiba

Miongoni mwa walioenda katika kituo cha afya cha serikali baada ya kuugua ama kuumia ndani ya miezi mitatu iliyopita, saba kati ya kumi (70%) walikutana na upungufu wa dawa na vifaa tiba. Hii ni idadi kubwa kuliko ilivyowahi kurekodiwa miaka iliyopita (53-62%).

Tatizo kubwa la pili lililojitokeza sana ni muda wa kusubiri: wananchi sita kati ya kumi (63%) walioenda kupata matibabu wanasema muda wa kusubiri ni mrefu sana.

Wananchi watatu kati ya kumi (29%) hawakukuta madaktari, na idadi sawa na hiyo walikuta huduma zikiwa ghali sana (28%) au wahudumu wa kituo cha afya hawakuwajali au kuwaheshimu (27%). Mgonjwa mmoja kati ya kumi (9%) walikuta vituo ni vichafu.

Upungufu wa dawa na vifaa tiba na kusubiri huduma kwa muda mrefu yamekuwa ni matatizo sugu katika sekta ya afya na idadi ya wananchi wanao kumbana nayo inaongezeka baada ya kushuka mwaka 2015. Kutokuwepo kwa madaktari na gharama za matibabu, kwa upande mwingine, vimeshuhudiwa na wagonjwa wengi baada ya kushuka mwaka 2016. Vilevile wagonjwa kutojaliwa na kuheshimiwa na wahudumu wa afya, au vituo kuwa vichafu, vimeendelea kubaki chini baada ya kushuka mwaka 2016.

Kielelezo cha 5: Kama ulitembelea kituo cha afya cha serikali kwa sababu ya kuugua ama kuumia ndani ya miezi mitatu iliyopita, je, ulikutana na tatizo lolote kati ya haya?



Chanzo cha takwimu. Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili
2015: Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015) ya kundi la kwanza
2014: Awamu ya 16 (Machi 2014) ya kundi la kwanza

Jambo la 5: Idadi ya watoto, wajawazito na wazee wanaopata matibabu bure imeongezeka tangu mwaka 2016

Watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee wenye miaka zaidi ya 60 wana haki ya kupata matibabu bure kwa mujibu wa sera ya matibabu bure kutoka katika vituo vya afya vya serikali. Hata hivyo, mwananchi mmoja kati ya watatu (35%) anasema watoto wenye umri chini ya miaka mitano walitakiwa kulipia matibabu. Vilevile, watu watatu kati ya kumi (28%) wanasema wajawazito walilipishwa matibabu na wananchi wanne kati ya kumi (37%) wanasema kuwa watu wenye miaka zaidi ya 60 hulazimika kulipia huduma hizo.

Hata hivyo, takwimu zinaonesha ongezeko dogo la idadi ya wagonjwa kutoka makundi haya wakipokea matibabu bure ukilinganisha na mwaka mmoja uliopita. Kwa watoto chini ya miaka mitano na wajawazito, ongezeko ni dogo sana, lakini kwa wenye miaka zaidi ya 60, idadi ya wanaopata matibabu bure imeongezeka tangu 2016 kutoka 49% hadi 56%.

Kielelezo cha 6: Mara ya mwisho ulipowasindikiza watu wafuatao kwenye kituo cha afya cha serikali, je, walipata matibabu bure, au walilipa?



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili

Jambo la 6: Wananchi 5 kati ya 6 wanasema walioumia kwenye ajali watibiwe hata kabla ya kupata fomu ya PF3

Linapokuja suala la watu walioumia kutokana na ajali ama ugomvi, wananchi watano kati ya sita (84%) wanasema wapatiwe kwanza matibabu kwenye vituo vya afya kabla ya kuhitajika kwa fomu ya PF3 kutoka polisi. Hili ni ongezeko dogo tangu mwaka 2016, ambapo wananchi nane kati ya kumi (79%) walisema hivyo.

Kielelezo cha 7: Nini mtazamo wako kuhusu mgonjwa (wa ajali; ugomvi; majeraha) kuhudumiwa katika kituo cha afya kabla ya kupatikana kwa PF3?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 9 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili

Miongoni mwa wale ambao waliwahi kupata ajali ama waliosaidiwa na rafiki ama familia baada ya kupata ajali, sita kati ya kumi (58%) walitakiwa na kituo cha afya kupeleka fomu ya PF3 kabla ya kupata matibabu. Moja kati ya maeneo matatu (32%) ambapo fomu ya PF3 ilienda kuchukuliwa, ilichukua zaidi ya saa nzima kupata fomu hiyo (haijaoneshwa kwenye jedwali).

Jambo la 7: Wananchi 3 kati ya 4 hawafahamu kazi za maafisa wa ustawi wa jamii

Kila serikali ya mtaa nchini ina kitengo cha ustawi wa jamii, ambacho huwepo kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali na ushauri (wa kijamii) kwa wananchi. Walipoulizwa kama wanafahamu kuhusu uwepo wa maafisa hao, wananchi watatu kati ya wanne (73%) walisema hawafahamu. Mwananchi mmoja kati ya kumi (11%) anafahamu uwepo wa maafisa wa ustawi wa jamii lakini hawafahamu kazi ya maafisa hao.

Mwananchi mmoja kati ya sita (17%) anafahamu kuhusu maafisa wa ustawi wa jamii na waliweza kutaja kazi zao ikiwemo kulinda haki za wanawake na watoto na kulinda makundi yaliyopo hatarini kama vile yatima na wazee.

Kielelezo cha 8: Je, unamfahamu mtumishi wa umma anayejulikana kama afisa wa ustawi wa jamii? Kama ndiyo, taja majukumu yake?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 19 (Mei 2017)

Mwananchi mmoja kati ya watano (20%) wanasema yupo afisa wa ustawi wa jamii kwenye wilaya yake, na idadi ndogo (1%) wanasema wameshaenda kwa afisa wa ustawi wa jamii kuomba msaada. Kwa wachache waliofanya hivyo, idadi kubwa (45%) ilikuwa ni kwa ajili ya kutafuta msaada wa kutatua migogoro ya ndoa na masuala ya malezi ya mtoto (haijaoneshwa kwenye jedwali).

Jambo la 8: Mwananchi 1 kati ya 4 ana bima ya afya

Bima ya afya huwasaidia wananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya. Mwananchi mmoja kati ya wanne (27%) wanasema wana bima ya afya, ongezeko kutoka mwananchi mmoja

kati ya watano (21%) miaka mitatu iliyopita. Kutokana na ongezeko la sasa, Tanzania huenda ikafikia kiwango cha kimataifa cha wananchi kufikiwa na bima ya afya ndani ya miaka 40 ijayo.

Kielelezo cha 9: Je, una bima ya afya au ya matibabu?

Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
2017: Awamu ya 19 (Mei 2017) ya kundi la pili
2016: Awamu ya 10 (Mei 2016) ya kundi la pili
2015: Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015) ya kundi la kwanza
2014: Awamu ya 16 (Machi 2014) ya kundi la kwanza

Kwa kuangalia watoa huduma wa bima, mwananchi mmoja kati ya nane (13%) anasema ana bima ya afya inayotolewa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), na mwananchi mmoja kati ya kumi (8%) anasema bima yao inatolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Kielelezo cha 10: Jina la kampuni au shirika linalotoa bima yako ya afya?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 19 (Mei 2017)

3. Hitimisho

Tanzania ina mengi ya kujivunia katika suala la matokeo ya uwekezaji kwenye sekta ya afya katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Watu wachache wanaugua malaria kuliko ilivyokuwa kipindi cha nyuma maambukizi ya virusi ya UKIMWI yamepungua na vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua vimeshuka kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, muhtasari huu unaonesha kuwa hatupaswi kuridhika, bali kuwekeza zaidi katika maboresho.

Vilevile, kwa kutazama viashiria chanya, inaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko la wananchi kwenda kupata matibabu kwanza kwenye vituo vya afya vya serikali tangu mwaka 2014-15.

Hii inaweza kuashiria kuwa vituo vya afya vimeongezeka na vinafikika kirahisi, na kwamba wananchi wamekuwa na imani na huduma zinazotolewa, au wananchi wamepata ufahamu zaidi juu ya umuhimu wa kupata vipimo sahihi kutoka kwa wataalamu wa afya. Pia imeonekana bayana kwamba muda wa kusubiri huduma katika vituo vya afya umepungua, na wananchi wengiwanasema hospitali zina vitanda, mashuka na vyandarua vya kutosha.

Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba si taarifa zote ni njema. Wagonjwa wanaostahili kupata matibabu bure bado wanahangaika kupata haki hiyo: karibu moja ya tatu ya watoto chini ya umri wa miaka mitano, wajawazito na wazee wenye miaka zaidi ya 60 huhitajika kulipia matibabu yao. *Sauti za Wananchi* ilipotoa takwimu kama hizi mwaka 2016, viongozi mbalimbali wa wizara husika walitoa maagizo ya kuwataka watumishi wa afya kutoyalipisha makundi haya. Takwimu hizi za mwaka huu zinaonesha matamko yale hayakutekelezwa ipasavyo.

Muhtasari huu pia umebaini kwamba wananchi wengi Zaidi wanataja upungufu wa dawa na vifaa tiba katika hospitali za serikali. Vilevile, tumeona kwamba mafaniko yaliyofikiwa kwenye suala la uwepo wa wahudumu wa afya na gharama za huduma ya afya mwaka 2016 sasa yanasuasua kutokana na wananchi wengi kulalamikia masuala haya.

Ni muhimu kwamba, mkakati wa serikali wa kutatua changamoto hizi sugu katika sekta ya afya, ulenge kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia bima za afya kutoka kwa watoa huduma wote ikiwemo Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na pia watoa huduma binafsi wa bima za afya kama vile Strategis na AAR. Hii inatokana na ukweli kwamba kumekuwepo na ongezeko la wananchi wenye bima yoyote ya afya – kwa kiwango kikubwa wakiwa na CHF au NHIF – lakini kiwango cha ongezeko ni kidogo sana. Jitihada kubwa za kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya zinahitajika.

Kwa kuhitimisha, ni vema tukakubali kwamba changamoto za vifaa tiba na rasilimali watu katika sekta ya afya nchini Tanzania lazima zipatiwe ufumbuzi wa kudumu. Utekelezaji wa kauli nzito na adhabu zinaweza kuisaida sekta hii lakini rasilimali za kutosha, mikakati mizuri yenye motisha kwa watumishi (wahudumu wote wa afya kuanzia madaktari mpaka maafisa unununzi) na mfumo wa uwazi na uwajibikaji wa manunuzi ya dawa na vifaa, vinahitajika kuhakikisha Tanzania yenye huduma bora za afya.